HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA KUZINDUA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2016/2017 - 2020/2021, CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI (IRDP) - DODOMA TAREHE 7 JUNI, 2016

Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb.), Waziri wa Fedha na Mipango;

Mheshimiwa Tulia Ackson Mwansasu (Mb.) – Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo hapa;

Mhe. Hawa Ghasia (Mb.) – Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti;

Mhe. Jordan Rugimbana – Mkuu wa Mkuu wa Dodoma;

Waheshimiwa Wabunge;

Mheshimiwa Jaji Mfawidhi wa Kanda ya Kati - Dodoma;

Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu wakuu mlioko hapa;

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Dodoma;

Washirika wetu wa Maendeleo;

Mkuu wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini –Dodoma pamoja na Wakuu wa Taasisi mliopo;

Wazee wetu pamoja na Viongozi wa Madhehebu ya Dini;

Viongozi wa Vyama vya Siasa;

Viongozi na Watendaji wa Serikali;

Wahadhiri na Wasomi wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP);

Wananchi

Wandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana.

SALAAM ALAIKUM!!
BWANA YESU ASIFIWE!!
TUMSIFU YESU KRISTO!!

Nitumie fursa hii kuwashukuru wote kwa kufika katika hafla hii fupi lakini muhimu ya **kuzindua Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano** 2016/2017 hadi 2020/2021. Mpango huu wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano una dhima ya *"Kujenga Uchumi wa Viwanda na Maendeleo ya Watu"*.

Napenda kutumia nafasi hii kupongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuamua kwamba tuzindulie Mpango wetu wa Pili wa Miaka Mitano katika Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini. Tumeona tuwashirikishe tangu mwanzo mipango yetu hii ya maendeleo kwa kuwa ni wadau muhimu. Serikali inatambua kuwa hapa kuna Wasomi ambao wanaandaliwa, ambao baadaye watakuwa na kazi kubwa ya kuelimisha jamii na kupeleka mipango ya maendeleo Vijijini.

Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana,

Awali napenda kueleza kuwa Uchumi wa Taifa letu umeendelea kukua vizuri katika kipindi cha muongo mmoja uliopita. Katika mwaka 2015, uchumi ulikua kwa kiwango cha asilimia **7.0** sawa na mwaka 2014. Shughuli za uchumi zilizoongoza kwa ukuaji huo zilikuwa ni: ujenzi asilimia **16.8**; habari na mawasiliano asilimia **12.1**; fedha na bima asilimia **11.8**; na uchimbaji madini na mawe asilimia **9.1**.

Kilimo ambacho ndicho uti wa mgongo wa uchumi na ambacho kinaajiri zaidi ya asilimia **70** ya watu wote nchini kiliendelea kukua kwa kasi ndogo ya asilimia **2.3** mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia **3.4** mwaka 2014. Sekta ya Viwanda nayo ilikua kwa asilimia **6.5** mwaka 2015 na ilichangia asilimia **7.3** ya Pato la Taifa.

Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana,

Pamoja na uchumi wetu kuendelea kukua, wananchi wetu wengi bado ni maskini. Kiwango cha kupungua kwa umaskini kati ya mwaka 2007 na 2012 ni asilimia **6.2** ikilinganishwa na miaka kumi na tano (2000-2015) iliyopita ambapo umaskini ulipungua kwa asilimia **4.6;** lakini zipo jitihada kubwa zinaendelea. Kuna ukweli kwamba kasi imeongezeka lakini bado asilimia **24** ya wananchi ambao ni takribani Watanzania **milioni 10.78** bado ni maskini. Serikali inaendelea kubuni na kutekeleza mikakati zaidi ya kuondoa umaskini, hasa katika kuongeza huduma za Jamii za elimu, afya,

maji, n.k, pamoja na kuimarisha huduma za Nishati Vijijini; huduma za kifedha Vijijini na kuimarisha miundombinu ya barabara, uchukuzi na mawasiliano.

Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana,

Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 ninaouzindua leo hii, kimsingi unalenga kuboresha maisha ya Watanzania walio wengi kwa kuhakikisha sekta zinazoajiri watanzania wengi na walio maskini kama vile Kilimo, Mifugo, Uvuvi na viwanda zinakua kwa kasi ya kuridhisha ili kuongeza fursa za ajira na kupunguza umaskini. Hivyo, utekelezaji wa Mpango huu ambao umefungamanisha maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu, unatazamiwa kujibu changamoto hii ya umaskini Tanzania. Matarajio yetu ni kwamba ifikapo mwaka 2025 tuwe tumejenga Nchi ambayo ina maisha bora kwa wote, yenye amani, umoja na utawala bora. Jamii inayojifunza na iliyoelimika; yenye uwezo wa kuzalisha na kuwa na ukuaji wa uchumi endelevu na wenye ushindani. Azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa shirikishi zaidi katika utekelezaji wa Mpango huu na kwamba uendelezaji wa viwanda ndio utakaotupa mafanikio makubwa katika mwelekeo huo. Msisitizo ni kuimarisha kufanya kazi zaidi.

Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana,

Napenda kuwakumbusha kuwa tangu kuanza kwa ubinafsishaji wa mashirika ya umma mwaka 1992, tulibinafsisha viwanda 106 kwa wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi. Lengo lilikuwa zuri la kuongeza ufanisi wa Viwanda husika hasa katika uzalishaji, kuvutia mitaji mikubwa ya kufufua viwanda husika, teknolojia mpya kuongeza ajira, kupunguza uagizaji wa bidhaa zinazoweza kuzalishwa hapa nchini na kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi. Wawekezaji katika **viwanda 34** wamefanya vizuri na viwanda vyao vinaendeshwa kwa ufanisi na hivyo kuongeza ajira na mapato ya Serikali. **Hawa ninawapongeza sana!** Hata hivyo,utafiti uliofanyika unaonyesha kuwa Wawekezaji katika viwanda 33 wameendesha kwa hasara. Aidha, wawekezaji katika **viwanda 39** vya bidhaa mbalimbali kama vile ngozi, chuma, korosho, zana za kilimo, sabuni na mafuta ya kupika wamevifunga au kutoviendeleza kabisa Viwanda hivyo, kinyume na makubaliano ya Mikataba ya mauzo baina yao na Serikali. Ninategemea Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Msajili wa Hazina itaendelea na zoezi la kuchukua hatua za kisheria kuvirejesha viwanda hivyo Serikalini ili kupitia Mpango huu wa Maendeleo tuangalie utaratibu mwingine ulio bora wa kuviendeleza. Kwa maana hiyo, Mpango huu pamoja na mambo mengine utajikita zaidi katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuendeleza viwanda vikubwa, vya kati, vidogo na vile vilivyobinafsishwa ili kuongoza fursa za ajira na kipato kwa wananchi wengi.

Msisitizo wa Serikali ni kutaka tujenge viwanda vingi ili kuwezesha kuzalisha ajira nyingi kwa Watanzania. Serikali ya awamu ya tano imetoa fursa zaidi kwa Watanzania wenye mitaji na wenye nia njema na walio makini kuwekeza kwenye viwanda. Vilevile, tunawakaribisha Wawekezaji wengine kutoka nje waje kutuongezea nguvu. Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji katika Viwanda ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu ya barabara, uchukuzi na mawasiliano na nishati ya umeme. Pia, tutaboresha Elimu na tutaweka mikakati ya upatikanaji wa fursa za kupata mitaji kwa Watanzania ili waweze kuwekeza katika sekta za Viwanda.

Mabibi na Mabwana,

Katika kutekeleza Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao utahitimishwa mwezi Juni, 2016, Serikali ilifanikiwa kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile: Ujenzi wa barabara mbalimbali za kiwango cha lami pamoja na madaraja ya Kigamboni, Malagarasi, Nangoo, Mbutu, Maligisu, Ruhekei na mengine katika barabara kuu na barabara za Mikoa. Aidha, Serikali imekamilisha Ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam (km **542**); Ujenzi wa mitambo ya kuchakata gesi katika maeneo ya Madimba na Songosongo; na Ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi vya Somanga – Fungu na Kinyerezi. Serikali pia imefanikiwa kutekeleza Ujenzi wa mitambo kufua umeme nchi nzima ikiwemo ya Kinyerezi I yenye uwezo wa kuzalisha **MW 150** iliyozinduliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Dkt. John Pombe

Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; pamoja na ujenzi wa njia za kusafirishia na kusambazia umeme na Utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini. Tunataka suala la mgao wa Umeme liwe ndoto katika Nchi yetu. Wizara ya Nishati na Madini inaendelea kuzungumza na Wawekezaji mbalimbali ili kuvutia wawekezaji katika sekta ya Nishati.

Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana,

Miradi mingine muhimu iliyokamilika ni utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (km 25,954) na kusambazwa katika mikoa 24 Tanzania Bara. Aidha, mradi wa Maji wa Ruvu Chini (Pwani) umekamilika pamoja na miradi mipya 1,160 ya maji ya vijiji 10 katika vijiji 1,206 yenye vituo 28,499 vya kuchotea maji katika Halmashauri 148. Miradi mingine katika maeneo ya kipaumbele ikiwemo miradi ya sekta za Huduma za Jamii, miundombinu, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu; na utalii, utawala bora huduma za kifedha na Biashara ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mabibi na Mabwana,

Miradi hii iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa, imeweka msingi mzuri wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Miaka Mitano ambao umejikita katika Maendeleo ya Viwanda Nchini. Ni kweli kwamba miradi hii imeleta majawabu kwa baadhi ya changamoto za uwekezaji nchini hususan kuweka Mazingira

Wezeshi ya Uendeshaji Biashara na Uwekezaji. Mpango huu unaozinduliwa leo unalenga kuimarisha mifumo ya kisheria ili iwe rafiki katika kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Vilevile, mpango huu utajikita zaidi katika kuimarisha miundombinu na huduma za msingi kwa uwekezaji, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa nishati ya umeme, miundombinu ya reli, barabara, bandari, usafiri wa anga, usafiri wa majini, miradi ya maji na TEHAMA.

Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana,

Kama mtakavyoona kwenye Vitabu vya Mpango huu kuna maeneo mbalimbali ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango huu. Kuna miradi iliyopewa sifa ya kuwa miradi ya kielelezo *(flagship projects)*. Miradi hii ni ile mikubwa na ambayo matokeo yake yanatarajiwa kuwa kichocheo au kuwezesha ufanisi wa utekelezaji na uwekezaji wa miradi mingine. Miradi hiyo ni kama vile mradi wa Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma; Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZA); Ujenzi wa Reli ya Kati na matawi yake kwa Kiwango cha *Standard Gauge* n.k. Serikali pia inatarajia kufufua Shirika la Ndege la Taifa kuanzia **mwezi Julai, 2016**. Naomba nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Mawaziri wanaosimamia Wizara zinazotekeleza miradi hii kujipanga upya na kuhakikisha kuwa malengo yaliyowekwa kwenye mpango huu yanafikiwa. Wakuu wa Mikoa ambao miradi hii ipo, ni lazima pia wahusike kikamilifu katika kuandaa mazingira wezeshi ili kuhakikisha kuwa wawekezaji na Serikali wanafikia malengo tarajiwa.

Mabibi na Mabwana,

Mtakubaliana nami kwamba ili Taifa letu liweze kusonga mbele na kufikia malengo ya maendeleo tunayoyakusudia tunahitaji kubadilika kifikra na kwa vitendo. Tunahitaji, kufanya kazi kwa bidii na maarifa na kuwa Wabunifu zaidi na kuacha kufanya kazi kwa mazoea. Nasisitiza watendaji wote wa umma hawana budi kufanya **kazi kwa bidii** na kuepuka kufanya kazi kwa mazoea. Sekta binafsi na Wananchi wote ni lazima wafanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo yao. Nasisitiza kuwa kila mtu akubali kubadilika kifikra na kwa vitendo na afanye kazi kwa tija na kuepuka kufanya kazi zisizo halali. Kila mtu afanye kazi **kwa ari na kujituma na kwa uaminifu ili tuweze kufikia malengo ya Mpango huu na tufikie malengo ya Dira ya 2025**. Serikali ya Awamu ya Tano imeahidi katika Ilani ya CCM tuliyoinadi kwa Wananchi wote kwamba tutapambana na Wakwepa kodi, tutapambana na wala rushwa na tutapambana na mafisadi. Serikali ya awamu ya tano inataka Wananchi wanyonge wajikwamue kiuchumi na kuondokana na Lindi la Umaskini. Tumeahidi kuwa tutatumikia Watanzania wote kwa ari kubwa na kwa uwezo wetu wote. Lengo letu kuu ni kutaka Watanzania wote wawe na maisha bora.

Mpango ninaouzindua leo ni nyenzo ya kutuelekeza kufikia nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Viongozi tuliopewa jukumu la kuongoza nchi hii tuna wajibu mkubwa kuhakikisha tunatekeleza malengo tuliyojiwekea kwa kujituma na kwa uaminifu. Baada ya miaka mitano tutapimwa na Watanzania tumefanikiwa vipi,

changamoto zipi tulikumbana nazo na hatua zipi tulichukua kukabiliana nazo. Ndiyo maana nasisitiza kuwa tunayo dhamana kubwa kwa Watanzania na hivyo ni muhimu kila mmoja wetu kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya “**HAPA KAZI TU**”.

Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana,

Ni dhahiri kwamba Mpango ninaouzindua una mahitaji makubwa ya rasilimali fedha na rasilimali watu. Serikali itahakikisha kuwa inaandaa mikakati ya kupata nguvu kazi yenye uwezo wa kutosha, ikiwa ni pamoja na kusomesha vijana wengi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi. Hivyo, sote kwa umoja wetu hatuna budi kuhakikisha kuwa fedha zinazohitajika zinapatikana kwa kuwahimiza Wananchi **kuendelea kulipa kodi kwa hiyari**, Serikali kutafuta vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha vyanzo vilivyopo. Aidha, Halmashauri nazo zinatakiwa kuendeleza juhudi hizi katika maeneo yao. Napenda kuwajulisha kwa katika mwaka wa Fedha wa 2016/2017 Serikali imeamua kuongeza fedha za Miradi ya Maendeleo kutoka **Asilimia 27** (2015/2016) hadi kufikia **Asilimia 40** (2016/2017) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. **Juhudi za kuongeza ukusanyaji wa mapato** kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango huu ni vyema ziende sanjari na usimamizi madhubuti wa matumizi ya fedha za Umma zinazopatikana pamoja na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana,

Ushiriki wa Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo ni muhimu katika utekelezaji wa Mpango huu. Hivyo, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wote wa maendeleo wa ndani na nje ili kutekeleza Mpango huu kwa ufanisi. Aidha, Serikali itaboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, kusimamia amani na utulivu nchini na utawala bora ikiwemo uwajibikaji na kupiga vita rushwa. Matarajio ni kwamba Wizara ya Fedha na Mipango itaandaa mkakati wa mawasiliano na kutayarisha Mpango huu kwa lugha nyepesi ili Wananchi wote waweze kuusoma, kuufahamu, kuuelewa na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake. Ninawaasa pia Wahadhiri na Wasomi wetu wa Vyuo Vikuu na wale wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini - Dodoma wausome vizuri Mpango huu na kuutumia katika masomo yao na kuishauri Serikali ili tuutekeleze vyema. Pia, Wasomi washiriki katika kuutekeleza Mpango huu ili tupate maendeleo ya haraka na kwa kasi. Nawashukuru Wadau wetu wa Maendeleo ambao wametuunga mkono katika kuandaa na kuweka mikakati ya kutekeleza Mpango huu.

Kabla ya kuhitimisha, napenda kuwashukuru Wananchi wote waliotoa maoni na Wadau wa Maendeleo, Wataalam mbalimbali pamoja na Waheshimiwa Wabunge waliotoa mchango wao wa mawazo ambayo yamewezesha kukamilisha maandalizi ya Mpango wetu huu. Mpango huu ni wetu hivyo tushirikiane wote kuutekeleza kikamilifu ili tupate maendeleo endelevu.

Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana,

Baada ya kusema haya machache ninaomba sasa nitumie nafasi hii kutamka kwamba nipo tayari **kuzindua Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021** kwa ajili ya utekelezaji

Asanteni sana kwa kunisikiliza!